

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



Jukwaa la Watumiaji Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Maadhimisho ya Siku ya Haki za Mtumiaji 2023 Kitaifa Kufanyika Jijini Mwanza

Dar es Salaam (07/03/2023). Maadhimisho ya Siku ya Haki ya Mtumiaji Duniani kitaifa mwaka 2023, yatafanyika mkoani Mwanza katika ukumbi wa Bwalo la Jeshi, huku yakiwakutanisha wadau mbalimbali ili kujadili masuala mtambuka yanayowahusu watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa na zisizodhibitwa hapa nchini.

Mgeni rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho hayo, yanayobebwa na kaulimbiu isemayo, “Kumjengea Uwezo Mtumiaji katika Matumizi ya Nishati na Nishati Mbadala,” anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. Adam Malima siku ya Jumatano tarehe 15/03/2023. Katika maadhimisho hayo, Mhe. Malima atahutubia makundi mbalimbali ya wadau.

“Hili tukio lenye tija kubwa kwa watumiaji na taasisi zinazohusika na utetezi wa watumiaji kote nchini. Siku hii, wadau hupata fursa ya kujadiliana kwa kina kuhusu hatima ya masuala mtambuka na kuja na mapendekezo ya namna bora ya kuboresha upatikanaji wa huduma na bidhaa zinanzokidhi viwango,” alisema ndugu Leo Ngowi, Mwenyekiti wa Jukwaa la Watumiaji Tanzania (TCF) na kuwataka wataanzania kuitumia siku hiyo, kutafakari mchango wao katika uboreshaji wa huduma na bidhaa wanazotumia.

Katika Maadhimisho hayo, kutakuwa na siku mbili za semina kwa wadau watakojengewa uelewa pamoja na mambo mengine, **kuhusu matumizi ya nishati na nishati mbadala** ikiwa ni moja ya jitihada za TCF, zinazolenga kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita, kuhamasisha matumizi ya nishati safi ili kukabiliana na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi.

Maeneo mengine yatakayotiliwa mkazo wakati wa semina hizo, ni pamoja na changamoto zitokanazo na huduma na bidhaa zinazotolewa kwa watumiaji na namna ya kukabiliana nazo, pamoja na kukuza uelewa wa watumiaji hao kuhusu Haki na Wajibu wao.



“TCF itatumia Maadhimisho hayo kuunga mkono jitihada za Serikali kufikia malengo namba 7 na 13 ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu, yanayosisitiza uchukuaji wa hatua za haraka katika kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake, sambamba na kuhamasisha upatikanaji wa nishati nafuu, ya uhakika, endelevu na ya kisasa hadi kufikia mwaka 2030,” alieleza ndugu Stella Lupimo, Kaimu Katibu Mtendaji wa EWURA CCC na kuongeza kuwa “Kwa mujibu wa takwimu za TFS za 2015, jumla ya ekari 372,871 za miti, hukakwa kila mwaka kwa ajili ya nishati ya kuni na mkaa,” hali inayotishia usalama wa mazingira na hivyo kuhitaji jitihada za haraka kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuuelimisha umma wa watazania kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi.”

Maadhimisho ya Siku ya Haki za Mtumiaji nchini Tanzania, huandaliwa na kuratibiwa na Jukwaa la Watumiaji, linaloundwa na Taasisi zinazowatetea watumiaji ambazo ni LATRA CCC, EWURA CCC, TCRA CCC, TCAA CCC, FCC na FCT kwa upande wa Tanzania bara, na kwa upande wa Zanzibar ZFCT na ZFCC.

Jukwaa la Mtumiaji Tanzania

Imetolewa la Mwenyekiti TCF
LATRA CCC
07 Machi, 2023

